

# MATOKEO YA KPSEA

Hatimaye baada ya ngoja ngoja ya muda, matokeo ya wanafunzi waliofanya mthani wa KPSEA ya-liweza kutolewa rasmi juma lililopita. Hii ni baada ya wanafunzi kujiunga na Gredi ya saba. Wanafunzi hao wanahimizwa kutia bidii ili kuboresha alama zao katika Sekondari ya Msingi.



## MTIHANI WA UFUNGUZI WA MUHULA

Mthani wa ufunguzi wa muhula wa kwanza wa mwaka 2024 uliweza kufanywa Jumatatu na Jumanne. Zoezi hili la siku mbili, ambalo hutumiwa na waelekezi kutathmini viwango vya wanafunzi wanapotoka nyumbani, ulishuhudia wanafunzi wa Gredi ya 5, 6, 7, na 8. Huku baadhi ya masomo kama vile Sayansi Kimu na somo la Elimu ya Afya yakifanywa kwa mara ya mwisho; kwani kwa sasa yameunganishwa na mengine.

## MISA YA KUFUNGUA MWAKA

Mnamo ijumaa mida ya saa tisa alasiri kuliweza kuandaliwa misa ya wanafunzi wa sekondari ya msingi ambao waliwakilisha shule nzima. Padre Reuben, anayehusika na watoto katika dekania ya Ruiru aliwari wanafunzi kuwa na shukrani kila wakati. Akizungumza katika hafla hiyo, padre aliwahimiza wanafunzi hao kujiunga na shirika la watoto la wamishonari (PMC). Aidha wanafunzi ambao hawajapokea sakramenti ya ubatizo walihimizwa kuhudhuria mafunzo kila Jumamosi kuanzia saa tisa kasorobo hadi saa kumi na moja za jioni.



## MICHEZO

Kundi la wapiga mbizi wa shule ya DePaul litakita kambi katika Taasisi ya MPESA Academy kwa makala ya mwaka huu ya mashindano ya mchezo huo. Waogeleaji kutoka madarasa tofauti wataandamana na waelekezi wao ili kupeperusha bendera ya shule yetu. Tunawatakia kila la heri.

## SHUGHLI ZIJAZO

Founders Day

(Siku ya Ukumbusho ya Baden Powell)

BTL Run for the Bibless

(Tafsiri ya Bibilia katika lugha za kiasili)

Students' Council Election

(Uchaguzi wa serikali ya wanafunzi)

Fun and Sports Day

(Siku ya michezo)

